

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE

08 JUNI, 2015



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE – TAREHE 08 JUNI, 2015

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha, 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU
YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA
MAENDELEO YA MAKAZI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha, 2015/2016.

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**160. MHESHIMIWA MCH. LUCKSON NDAGA
MWANJALE (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Ujenzi wa Stendi na Barabara zake katika mji mdogo wa Mbalizi ulikuwa ni sehemu ya ahadi za Mhe. Rais wakati wa Kampeni za Mwaka 2010:-

Je, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi hiyo.

**161. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI
KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Jimbo la Mpanda Vijijini lina shule za Sekondari saba (7) ambazo ziko katika Kata ya Karema, Ikola, Kabungu, Katuma, Mishamo na Mpanda ndogo lakini shule hizo zina upungufu mkubwa wa walimu:-

- (a) Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kutosha katika shule hizo za Mpanda Vijijini;
- (b) Je, Serikali haioni kuwa kutokuwa na walimu kumesababisha kushuka kwa elimu na hivyo kuwafanya wanafunzi kufeli mitihani.



WIZARA YA NISHATI NA MADINI:



**162. MHESHIMIWA MOZA ABEDI SAIDY (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Katika miradi ya ujenzi wa barabara, Kampuni kutoka nje zimekuwa zikipasua miamba ambayo mingine ina madini:-

Je, Serikali huwa inafuatilia hatua kwa hatua kubaini madini hayo ili yaweze kunufaisha Serikali na Wananchi kwa ujumla.

WIZARA YA FEDHA:

163. MHESHIMIWA ENG. ATHUMAN RASHID MFUTAKAMBA (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, ni wapi patafaa Duniani kwa ajili ya kuwekeza fedha za ziada (sovereign wealth fund) tutakapoanza kuuza Petrol na Gesi nchini na Duniani ili uchumi wetu kuanzia mwaka 2020 usiyumbe.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

164. MHESHIMIWA SUSAN ANSELM LYIMO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Suala la Mikopo ya Elimu imeendelea kuwa na changamoto kila mwaka, hali iliyopelekea kuundwa kwa Tume chini ya Uenyekiti wa Prof. Maboko:-

Je, matokeo ya Tume hiyo yakoje na ni kwa kiasi gani ilitatua changamoto hizo.

**165. MHESHIMIWA DKT. DALALY PETER
KAFUMU (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Mwaka 2005 Serikali iliahidi kujenga Chuo cha Ufundi VETA katika Wilaya ya Igunga ili kuwapatia Vijana mafunzo ambayo yatawasaidia kujiajiri:-

Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini.

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

**166. MHESHIMIWA MTUTURA ABDALLAH
MTUTURA (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Mara nyingi Serikali imekuwa ikitangaza kupigwa marufuku kusambaza, na kuuza baadhi yadawa za binadamu zinazodaiwa kuwa na madhara ya kiafya licha ya kuwa dawa hizo zilipata kibali cha kutumika nchini miaka kadhaa huko nyuma:-

- (a) Kwa nini Serikali isijiridhishe mapema kabla ya kuruhusu dawa hizo kutumika;
- (b) Je, Serikali imefanya utafiti kuona kama Wananchi waliotumia dawa hizo kwa muda mrefu wamepata madhara yoyote.

WIZARA YA UJENZI:

167. MHESHIMIWA IGNAS ALOYCE MALOCHA (KWELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-
Kukosekana kwa daraja katika Mto Momba linalounganisha Wilaya ya Sumbawanga Vijijini na Wilaya ya Momba kati ya Vijiji vya Kilyamatundu na Kamsamba ni tatizo sugu kwa Wananchi wa maeneo hao; mwaka 2013/2014 Serikali ilitenga shilingi Bilioni


- Mbili na mwaka 2014/2015 ilitenga tena shilingi Bilioni Mbili lakini hadi sasa ujenzi wa daraja hilo bado haujaanza:-

- (a) Je, ni hatua gani imefikiwa katika ujenzi wa daraja hilo;
- (b) Je, ni lini ujenzi huo utaanza rasmi na kukamilika;
- (c) Je, ni kiasi gani cha fedha kinahitajika ili kukamilisha ujenzi wa daraja hilo.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.



**DODOMA
08 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**